# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

## MUHTASARI WA RIPOTI YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI (PAC) YA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MWAKA 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** kwa heshima na utii wa hali ya juu natanguliza shukurani zangu kwa Mwenyezi Mungu, Bwana wa viumbe vyote, ambae ametujaalia uhai, afya njema na taufiki ya kuweza kukutana hapa leo, kwa lengo la kutekeleza majukumu yetu ambayo Waheshimiwa Wananchi wametutuma tuje kuyatekeleza hapa Barazani kwa niaba yao.

**Mheshimiwa Spika**, kwa heshima kubwa nimesimama mbele ya Baraza lako Tukufu kwa ajili ya kuwasilisha Muhtasari wa Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) kwa mwaka 2022/2023 kama ambavyo Kanuni ya 109(15) ya Baraza lako Tukufu, Toleo la mwaka 2020 inavyoelekeza.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Kamati ya PAC ilizifanyia kazi Ripoti tatu za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Heabu za Serikali zilizowasilishwa hapa Barazani na Waziri Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Mheshimiwa Haroun Ali Suleiman kwa niaba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kama inavyoelekezwa na Kifungu cha 112 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ambazo ndio nyenzo kuu za utekelezaji wa majukumu ya kazi za Kamati hii kama yalivyoainishwa katika Jadweli la Kwanza lililoundwa chini ya Kanuni ya 107 ya Kanuni zetu za Kudumu.

**Mheshimiwa Spika,** Ripoti ambazo Kamati ya PAC imezifanyia kazi ni hizi zifuatazo:-

1. Ripoti ya Ukaguzi Maalum Unaohusu Utekelezaji wa Maagizo ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi wakati wa kuwaapisha Viongozi Wakuu uiliyojumuisha:-

    a) Ripoti ya Ukaguzi Maalum Kuhusu Malipo ya Wazee ya Pencheni Jamii kwa Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2020;

b) Ripoti ya Ukaguzi Maalum kuhusu ufanisi wa utekelezaji wa Mradi wa Kilimo cha Pilipili Hoho kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2020;
c) Ripoti ya Ukaguzi Maalum kuhusu Ununuzi wa Mchele na Mbolea kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2020; na
d) Ripoti ya Ukaguzi Maalum kuhusu Ukodishwaji wa Mashamba ya Mikarafuu.

2. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021; na
3. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (CDF) kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2019 hadi 2020.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya PAC kwa kipindi hicho haikuweza kuzifanyia kazi Ripoti zote Sita zilizowasilishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika Mkutano wa Nane wa Baraza la Kumi katika kikao cha tarehe 13 Septemba, 2022 ikiwemo Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Miradi ya Maendeleo na Ukaguzi wa Mifumo ya Tehama. Hata hivyo, Ripoti hizo zinatarajiwa kufanyiwa kazi katika mzunguko ujao wa kazi za Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya PAC imeanza kuifanyia kazi Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021 kwa kukamilisha uchunguzi wake katika Wizara nne (4) pamoja na Idara zake kama inavyojionesha hapa chini:-

1. Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;
2. Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo;
3. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali;
4. Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ; na
5. Baadhi ya Taasisi za Wizara ya Afya zikiwemo Wakala wa Mkemia Mkuu na Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya PAC inaendelea kuifanyia kazi Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021 kwa baadhi ya Wizara na Taasisi zake ambazo bado Kamati haijakamilisha uchunguzi wake. Miongoni mwa Wizara hizo ni Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Unguja pamoja na baadhi ya Taasisi za Wizara ya Afya Unguja. Aidha, kutokana na muda kuwa mchache ukilinganisha na hoja zinazohitaji kufuatiliwa na kuchunguzwa, baadhi za Wizara ambazo zimeainishwa katika Ripoti ya Ukaguzi wa Serikali Kuu bado Kamati haijaanza kuzifanyia kazi isipokuwa imejipanga kutekeleza ukaguzi wake katika ratiba ya kazi zake zijazo.

**Mheshimiwa Spika,** ili kufanikisha ukaguzi wa Kamati yetu, njia kuu tatu zifuatazo zilitumika:

1. Kufanya vikao vya mahojiano na Maafisa Masuul, Watendaji mbali mbali wa Serikali pamoja na Wajumbe wa Kamati za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo;
2. Kukagua nyaraka na vielelezo vilivyohusika na hoja zilizojadiliwa (Compliance Audit); na
3. Kufanya ziara katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba ili kuweza kujiridhisha na kuthibitisha juu ya utekelezaji unaohusika, na kuangalia iwapo matumizi ya Serikali yamezingatia thamani halisi ya fedha (Value for Money Audit).

**Mheshimiwa Spika,** tathmini ya Kamati ya PAC inaonesha kuwa Wizara na Taasisi za Serikali zimekuwa zikichukua hatua kurekebisha dosari za kiutendaji zinazobainishwa na vyombo vya Uchunguzi na Udhibiti wa Hesabu za Serikali ikiwemo Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Kamati ya PAC. Hivyo, kipo kiwango cha kuimarika kwa nidhamu ya matumizi ya rasilimali za umma katika utendaji wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Katika utekelezaji wa kazi za Kamati yetu kwa mwaka 2022/2023, Kamati ya PAC ilifanikiwa kuibua kasoro kadhaa za jumla ambazo zimeelezewa kwa undani katika Ripoti yetu, miongoni mwa kasoro hizo ni pamoja na:-

1. Kukosekana kwa mashirikiano baina ya Watendaji wa Wizara na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali hususan katika kipindi cha ukaguzi na wakati wa uwasilishaji wa vielelezo au nyaraka;
2. Usimamizi mbaya wa fedha za Umma hususan zinazohusiana na Mapato na Matumizi;
3. Uwekaji mbaya wa kumbukumbu na vielelezo vya Mapato na Matumizi;
4. Upotevu na Matumizi mabaya ya fedha za Serikali;
5. Upatikanaji wa fedha usiolingana na Mpango au Bajeti ya Wizara husika;
6. Mtumizi mabaya ya fedha za Serikali;
7. Uwepo wa madeni ya muda mrefu;
8. Kukosekana kwa mashirikiano baina ya Kamati na Watendaji wa Wizara; na
9. Ukiukwaji wa Sheria, Kanuni na taratibu za Fedha na Ununuzi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya PAC imebaini kuwa wakati Wakaguzi kutoka Ofisi ya Mthibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wanapofika katika Wizara za Serikali au Taasisi zake kutekeleza majukumu yake ya Kikatiba, Wakaguzi hukumbana na mazingira magumu ya kutopatiwa vielelezo au maelezo sahihi yanayothibitisha uhalali wa Mapato au Mtumizi yaliyotekelezwa na Watendaji wa Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya PAC imekutana na uhalisia huo ilipokuwa ikichunguza hoja za Wizara ya Kilimo, Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii, Chuo cha Mafunzo, Kikosi cha Valantia Pemba (KVZ) pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango Pemba.

**Mheshimiwa Spika,** kushindwa kwa watendaji wa Serikali kuwapatia ushirikiano Wakaguzi hususan wanapohitaji vielelezo au majibu sahihi hupelekea kujitokeza kwa hoja nyingi katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambazo kuihalisia hazikutakiwa kujitokeza.

**Mheshimiwa Spika,** Lakushangaza, wakati Mkaguzi anafipoka katika Taasisi za Serikali huelezwa kwamba vielelezo au majibu hayapo lakini ikifika Kamati ya PAC, vielelezo vingi vinakuwepo ambavyo vinatosheleza kuzuia hoja kuingizwa katika kitabu cha Ripoti. Kwa mnasaba huo, Kamati yetu inaiomba Wizara ya Fedha na Mipango kuwapatia elimu Maafisa Wahasibu, Maafisa Wanunuzi na Wakaguzi wa Ndani ili wawe tayari kukabiliana na hoja za Mdhibiti kama ni moja kati ya majukumu yao makuu ya kazi zao kwa lengo la kuinusu Wizara na hoja zisizo za lazima. Aidha, Kamati inawataka Maafisa Masuul kushiriki ipasavyo katika vikao vya Mkaguzi kwani yeye ndio anaefahamu mambo mengi ya Ofisi husika.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na maumbile na mazingira yaliopo katika Vikosi vyetu vya SMZ hususan katika utekelezaji wa majukumu yao ambao huzingatia zaidi usiri, nidhamu na heshima maalum ya kazi, Kamati yetu imebaini hali hiyo huchangia zaidi kwa Watendaji wa Mdhibiti kukosa ushirikiano unaotakiwa. Hivyo, Kamati ya PAC inaiomba Ofisi ya Mdhibiti kuandaa Watendaji maalum watakaokwenda kufanya ukaguzi katika Vikosi hivi. Aidha, Watendaji wa Mdhibiti wanapofika katika Vikosi hivyo wakutane na Makamanda Wakuu au Wasaidizi wao Wakuu kwa vile ndio wenye kutambua mambo ya ndani ya Vikosi hivyo na ndio wenye mamlaka ya kukisemea Kikosi husika.

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, ni vyema Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Taasisi zake zinazowasimamia Wahasibu, Wakaguzi wa Ndani pamoja na Maafisa Manunuzi kutoa kipaumbele maalum cha kuwapatia Mafunzo Makamanda wanaoshughulikia masuala ya fedha na ununuzi ili kuwaongezea taaluma na ujuzi utakaowasaidia kutekeleza vyema Sheria na taratibu za fedha na Manunuzi.

**Mheshimiwa Spika,** zinazohusiana na fedha zikiwemo Kamati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake ya Kikanuni katika Baraza la Mitihani Zanzibar, ilifanikiwa kubaini kwamba kuna jumla ya shilingi zisizopungua bilioni 3 hazikuwa na vielelezo vinavyoeleweka ili kuthibitisha uhalali wa matumizi yake. Kamati ya PAC, imemshauri Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kulifuatilia kwa undani suala hili ili Serikali itambuliwe fedha hizo zimetumika kwa uhalali gani.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inampongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Mheshimiwa Lela Mohamed Mussa kwa kuanza kuchukua hatua stahiki za kumuelekeza Mkaguzi Mkuu wa Ndani kuunda Kamati Maalum ya kufanya Ukaguzi Maalum kuchunguza matumizi ya shilingi Bilioni 3 zilizotumika katika mwaka 2020/2021. Hatua hiyo ni ya busara itakayoweza kutupatia majibu na hatua stahiki za kutekelezwa dhidi ya wafanyakazi wote watakaogundulika wamehusika na ubadhirifu wa matumizi ya fedha za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Fedha hizo ni nyingi ambapo sio busara hata kidogo kwa nchi changa kama hii kuziachia ziende na maji bila ya Serikali yetu sikivu kuwawajibisha wachache wasiopenda manufaa ya waliowengi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeifanyia uchunguzi Ripoti ya muda mrefu kuhusiana na utekelezaji wa Mradi wa Pilipili Hoho. Kamati ya PAC imebaini kwamba Mradi huo uliolenga kuwasaidia vijana ili waweze kupata kipato cha kujiendesha kimaisha ambao ulitekelezwa bila ya kupatikana tija kwa vijana wala kwa Serikali yetu kwani jumla ya shilingi 183,000,000 kati ya fedha zote shilingi 560,000,000 zimepotea kutokana na uzembe wa Watekelezaji Mradi huo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini Mradi wa kilimo cha Pilipili hoho katika eneo la Pangatupu ulitekelezwa bila ya kufuata maelekezo ya utafiti uliofanyika. Kwa nia njema, Serikali yetu kabla ya kuanza Mradi wa Pilipili hoho, iliamua kufanya utafiti (study) iliyokuja na mapendekezo ya maeneo ambayo yanaweza kulimwa Pilipili hizo na kumea vizuri likiwemo eneo la Mihulani, Finya na Pujini. Matokeo yake, wafanyakazi wa Wizara ya Biashara waliamua kuutekeleza Mradi huo katika eneo la Pangatupu, eneo ambalo ni la kichanga na huwa linakaa maji ya mvua na halikupendekezwa na Utafiti uliofanywa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya PAC inasikitika kuliarifu Baraza Lako Tukufu kuwa lengo na tija iliyokusudiwa katika Mradi huu haijafikiwa na badala yake fedha za Serikali zinaonekana kutumiwa vibaya na kupotea kwani Pilipili hizo zilifunikwa na maji ya mvua na kufa. Kamati inapendekeza kwamba wale wote waliohusika na utekelezwaji wa Mradi katika eneo lisilostahiki wachunguzwe na ikithibitika, sheria ichukue mkondo wake.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Mradi uliotekelezwa eneo la Bambi, Kamati imekuta hakuna miundombinu ya maji iliyopo wala Pilipili zilizolimwa katika eneo hilo. Lakushangaza, Mradi ulibakisha mgogoro wa matumizi ya eneo lililokuwa likitumika kwa kilimo baina ya wamiliki wa eneo hilo na baadhi ya vijana waliokuwa wakinufaika nalo. Kamati yetu imeitaka Wizara ya Biashara kuumaliza mgogoro huo kwa amani. Aidha, mambo mengine yaliyobainika yanapatikana kwa urefu katika Ripoti yetu ambayo Waheshimiwa mmepatiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu ilipata nafasi ya kuchunguza Ripoti ya Mdhibiti kuhusiana na kutokupokelewa kwa Tani 740 za mbolea (UREA) kutoka kwa Kampuni ya Pensel Trading Limited iliyosajiliwa nchini China. Kamati ya PAC imebaini kuwa Wizara ya Kilimo haikutekeleza majukumu yake kwa uweledi na kupelekea fedha za Serikali kutumika vibaya na Mbolea iliyokusudiwa kununuliwa kwa thamani ya fedha hizo hazikufika Serikalini wala kwa wakulima ambao ndio wanufaika wakubwa. Hili lilitokana na kutokutekelezwa kwa Mkataba wa ununuzi wa Mbolea hiyo ambao ulikuwa unaelekeza wazi kwamba Mnunuzi atalipwa fedha zake baada ya kuisafirisha na kukabidhi vielelezo vyote vya mbolea ikiwemo 'bill of landing'.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya PAC imebaini kuna ufujaji na upotevu mkubwa wa fedha za Serikali. **Tunaviomba vyombo vya Serikali na Taasisi zinazohusika na uchunguzi, kufuatilia kwa karibu upotevu wa fedha hizo za Serikali kwa Wizara ya Kilimo.**

**Mheshimiwa Spika,** lakusikitisha na kuhuzunisha Mnunuzi huyo amelipwa fedha zote kabla ya kuwasilisha chochote. Matokeo yake, mbolea hadi hivi leo haijafika na wala haitowasilishwa tena badala yake Mnunuzi atarudisha fedha kidogo kidogo, jambo ambalo sio matakwa na makubaliano ya Serikali. Kutowasilishwa kwa mbolea hiyo kumepelekea mipango ya Serikali kutotekelezeka kama ilivyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** wakati Kamati inafuatilia majibu ya hoja hizo, inasikitika kusema haikupata mashirikiano kabisa kutoka kwa aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo pamoja na Muhasibu wake ambapo kila Kamati ilipokutana na Wizara hiyo, hawakushiriki vikao vya Kamati. Kamati ya PAC ilipata mashaka kwa Afisa Masuul wa Wizara ya Kilimo kususia kushiriki vikao vya Kamati ya PAC, kufanya hivyo sio kosa pekee kwa mujibu wa Sheria ya Fursa, Kinga na Uwezo wa Wajumbe bali pia ni ukosefu wa nidhamu kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya PAC imefanikiwa kukamilisha ukaguzi wake katika Ripoti ya Ukaguzi Maalum kuhusiana na Ukodishwaji wa Mashamba ya Mikarafuu Kisiwani Pemba. Kiujumla, Kamati kwa masikitiko imegundua fedha ya Serikali zimepotea. Kamati ilibaini madudu mengi yaliyofanyika katika mchakato mzima wa utafutaji mashamba yaliyokuwa hayatambuliki, wakati wa minada na zaidi wakati wa ulipaji fedha za ukodishwaji Mashamba na fedha za Kifutajasho.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imegundua kwamba zaidi ya jumla ya shilingi milioni 380 zimepotea kwani hadi Kamati inakamilisha uchunguzi wake zilikuwa hazijalipwa na Wakulima tangu mwaka 2017 zoezi la uchumaji wa mzao mkubwa wa Karafuu lilipofanyika. Lakushangaza zaidi, Kamati haikuridhishwa na utendaji wa Wizara ya Kilimo kwa kutokuwa na mikakati imara itakayohakikisha madeni hayo yanalipwa na kuendelea kufuatiliwa kwa karibu ili yaweze kulipwa.

**Mheshimiwa Spika,** lakufurahisha ni kwamba Ripoti ya Mdhibiti imeainisha mpaka Wakulima na kiasi cha fedha wanachodaiwa. Hivyo, tunaiomba, Wizara ya Kilimo kuyafuatilia madeni hayo na ikithibitika wawafungulie Wadaiwa hao shauri la Madai ili kuwalazimisha kukamilisha madeni yao pamoja na gharama nyengine za usumbufu ambayo Serikali imeingia.

**Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa mambo mengine ya msingi ambayo yalibainika na Kamati katika ukaguzi wa Ripoti ya Ukodishwaji wa Mashamba ya Mikarafu ni pamoja na:-

1. Zoezi la ukodishwaji mashamba ya mikarafuu lilikabiliwa na utumiaji mbaya wa madaraka kwa baadhi ya watendaji wa Serikali kujilimbikizia mali za umma;
2. Kuna baadhi ya mikataba haikutiwa saini na wakodishwaji na kupelekea wasiwasi kuhusu uhalali wa ushahidi huo;
3. Kuna baadhi ya wakulima walikodishwa mashamba lakini hawajawahi kusaini hata mkataba mmoja;
4. Ukodishwaji wa baadhi ya mashamba ulifanywa kwa kujuwana kwa kutumia msemo **'linatundikwa'** kwa maana kwamba shamba hilo halijafikia bei katika mnada na baadae watu wanazunguka nyuma na kukodishwa kwa bei ya chini kabisa;
5. Kuna baadhi ya Wakodishwaji wanadaiwa fedha nyingi ambazo hawajalipa kutokana na kutosimamiwa ipasavyo; na
6. Kuna baadhi ya wakodishwaji wameonakana wanadaiwa madeni kidogo katika kitabu wakati uhalisia wanadaiwa madeni makubwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Idara Maalum za SMZ, Kamati ya PAC imebaini kwamba, Vikosi hivyo huwa vinawekewa kiwango kikubwa cha ukusanyaji mapato kinyume na uhalisia na uwezo wa vyanzo wanavyovitegemea. Matokeo yake, hushindwa kufikia malengo ya makusanyo kama ilivyopangwa. Aidha, kwa maumbile ya shughuli za Vikosi vyetu, vinahitaji kuwezeshwa kupitia vyanzo vyao kwa kuruhusiwa kubakisha kiwango fulani cha mapato wanayoyakusanya na sio kuwasilisha mapato yote hazina.

**Mheshimiwa Spika,** ili Vikosi vyetu viweze kujitegemea, ni busara Wizara ya Fedha na Mipango ikalitekeleza hilo kivitendo kwani Vikosi kama cha JKU, Chuo cha Mafunzo na KMKM huwa na mifugo (wakiwemo kuku na Ng'ombe) wanayoiendeleza. Kuyachukua mapato yote bila ya kubakia chochote huwawia vigumu kulipia gharama nyingi za uendeshaji wa mifugo hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na utendaji mzuri unaofanywa na Vikosi vyetu vya SMZ hapa Zanzibar. Kamati ya PAC ilipitia kwa undani hoja nambari 6.3.2.14 na 6.3.6.5 za Kikosi cha JKU na KZU zinazohusiana na uhamisho wa kikazi kwa Wapiganaji wa Vikosi hivyo. Kamati yetu imebaini vikosi hivyo vinakabiliwa na changamoto ya mgongano wa Kikanuni ambao

unakwaza utendaji wa majukumu yao. Hili limetokana na kutofautiana kwa maslahi yaliyoelezwa katika Kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014 na Kanuni ya Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ.

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 89(1)(2)(3) ya Utumishi wa Umma inaeleza kwamba kulipwa Posho la Usumbufu litakalokuwa sawa na posho la siku saba pamoja na usafiri wa ndani wa kufidia usumbufu atakaoupata katika kutekeleza amri hiyo ya uhamisho lakini pia atastahiki kugharamiwa uhamishaji wa familia na mizigo yake, wakati na Kanuni ya 60(g) cha Kanuni ya Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ kinaeleza kulipwa stahiki posho la usumbufu ambalo lita fungamana na uhamisho wa kutoka Unguja kwenda Pemba au kinyume chake la asilimia 25 ya mshahara".

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mnasaba huo, ni vyema kwa Taasisi husika zikapendekeza kufanyiwa marekebisho kwa Kanuni hizo ili ziwe rafiki kwa watumishi na zisiwe na tofauti yoyote. Kubakia hivyo, kunaonesha upande mmoja unanufaika zaidi na mwengine unadhulumiwa.

**Mheshimiwa Spika,** sote ni mashuhuda wa juhudi ambazo Serikali yetu inazichukua katika kuhakikisha Watumishi wanapatiwa ipasavyo stahiki zao kama alivyoelekeza Rais wetu Mpendwa kwamba Watendaji Wakuu wa Serikali wahakikishe wanatoa kipaumbele kulipa stahiki hizo ikiwemo fedha za likizo. Hata hivyo, kuna baadhi ya Wizara utekelezaji wake unasuasua kwa madai ya upungufu wa fedha wakati ukifanya tathmini utagundua wanaodai ni Wafanyakazi wa ngazi za chini pekee na sio vyenginevyo.

**Mheshimiwa Spika,** Hadi Kamati ya PAC inakamilisha uchunguzi wake, jumla ya shilingi 56,000,000 ni deni lililobakia la posho za likizo wanazodai wafanyakazi wa Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo ambapo shilingi 30,000,000 zimelipwa kutoka jumla ya shilingi 86,000,000 zilizokuwa zikidaiwa na wafanyakazi wake. Kamati yetu imeisisitiza Wizara kuandaa Mpango Maalum wa ulipwaji wake pamoja na kutoa kipaumbele katika utekelezwaji wa Mpango huo muhimu.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza uchunguzi wake kwa Wizara ya Fedha na Mipango Pemba, Kamati ya PAC haikuridhishwa na imesikitishwa sana na kitendo cha Watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango Pemba kuidanganya Kamati ambapo ni sawa na kulidanganya Baraza lako Tukufu wakati ikitekeleza majukumu yake ya Kikanuni ilipokuwa inapitia hoja nambari 6.4.1.5 ya Ripoti ya Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu inayohusiana na kukosekana kwa uthibitisho wa safari kwa malipo ya fedha za safari kikazi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inadhubutu kueleza hayo kufuatia Watendaji wa Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba wa Wizara hiyo kudai kwamba wafanyakazi wake walitumia jumla ya shilingi 42,032,500 kwa ajili ya safari

za kikazi Unguja. Kamati imeshindwa kulithibitisha hilo baada ya kufuatilia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kufuatia kuiandikia barua ya tarehe 31 Oktoba, 2022 na kujibiwa kwa barua ya tarehe 11/11/2022 ambayo iliwasilisha nakala ya daftari la Wasafiri (Manifest) kwa siku na muda wa safari ambao uliainishwa katika barua hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa bahati mbaya na kwa masikitiko makubwa, Kamati ya PAC imegundua kwamba hakukuwa na jina hata la Mfanyakazi mmoja kati ya wale waliokuwemo katika barua walionekana katika daftari hilo kuwa walisafiri katika siku, muda na ndege husika licha ya Wizara kuionesha Kamati nakala za tiketi za wafanyakazi hao. Kwa mnasaba huo, Kamati ya PAC inatamka kinywa kipana kwamba kuna upotevu wa fedha hizo kwani kielelezo pekee kinachoweza kuthibitisha kwamba Mtendaji amesafiri ni kuwemo katika daftari hilo na sio kuwa na tiketi kitu ambacho kinaweza kupatikana kwa Mawakala wa ndege wasiokuwa waaminifu.

**Mheshimiwa Spika,** kwenye suala hili, tunashauri Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kuchukua ipasavyo hatua za kinidhamu dhidi ya wale wote waliohusika na kadhia hii ikiwemo kuzirudisha fedha za umma zilizopotea pamoja na hatua nyengine anazoona zinafaa kwa mujibu wa sheria.

**Mheshimiwa Spika,** tunawashauri Watendaji wote wa Serikali kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu ili wananchi waliowengi waweze kunufaika na huduma wanazozitoa kwa niaba ya Serikali yetu lakini suala la kuzitumia fedha za Serikali kinyume na utaratibu naamini haliungwi mkono sio na Kamati zako tu bali hata Baraza lako Tukufu.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kufuatilia hoja za Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi, Kamati ya PAC imebaini kuwa baadhi ya Watendaji wake waliokuwa wakikusanya mapato hawakuwa na sifa za kufanya kazi hizo kwani badala ya kazi hizo kutekelezwa na watendaji wenye utaalamu wa masuala ya fedha ilikuwa ikifanywa na Wakaguzi wa Machinjio. Hali hiyo, imepelekea kuikosesha mapato Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kama hilo halitoshi, Kamati yetu imegundua kwamba kuna baadhi ya Wafanyakazi wa Wakala hawakuwa waaminifu katika ukusanyaji waliokuwa wakiufanya kwani Kamati yetu imegundua kuwepo kwa tofauti ya fedha shilingi 970,274 iliyorikodiwa kwenye daftari la kumbukumbu za mapato kuwa tofauti na fedha zilizorikodiwa kwenye stakabadhi. Kwa mnasaba huo, kulikuwa na fedha ambazo zinaishia katika matumbo ya Watendaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya PAC haikuridhika na utendaji mbaya wa baadhi ya Wafanyakazi wa Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi na kupendekeza kwamba kuna kila sababu kwa Serikali kupitia vyombo vyake vya uchunguzi kufualitia, kuchunguza zaidi na hatimae kuwachukulia hatua za kisheria wale waliohusika na kadhia hiyo ili haki iweze kutendeka

na kutoa funzo kwa Watendaji wengine kwamba vyombo vya kusimamia upotevu wa Fedha za Umma vipo na vinatekeleza majukumu yake kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika,** sote tunaelewa kwamba nchi yetu inafanyakazi kwa kuzingatia misingi ya Utawala Bora, Haki za Binadamu na Utawala wa Kisheria. Kamati ya PAC inaipongeza sana Serikali yetu kwa kufuata ipasavyo dhana hizo. Hata hivyo, Kamati yetu imepata changamoto katika utekelezaji wa majukumu yake ya kiuchunguzi kwa Watendaji wa Wizara za Serikali kudai kwamba baadhi ya Watendaji wanaohusika na hoja zilizoibuliwa na Mdhibiti, kuwa tayari wameshaitwa na ZAECA kwa hatua za kiuchunguzi. Sambamba na hilo, Kamati imeelezwa alipopita Mkaguzi baadhi ya nyaraka zilichukuliwa na ZAECA. Hali hiyo ilipelekea hoja nyingi kujitokeza katika Kitabu cha Mdhibiti.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mantiki hiyo, ni vyema kwa Taasisi za uchunguzi zinapohitaji kupatiwa nyaraka kuwepo na utaratibu wa kukabidhiana nyaraka hizo kwa wakati wote wanaochukua na kurudisha ili kuondosha kuoneshana vidole itakapotokezea upotevu wa nyaraka au kielelezo husika.

**Mheshimiwa Spika,** masuala hayo yamejitokeza Kamati ilipokutana na Makamanda wa Jeshi la Kujenga Uchumi, Chuo cha Mafunzo, Kikosi cha Zimamoto na Uokozi pamoja na Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na kwamba Sheria ya ZAECA haikuweka kikomo cha utekelezaji kazi zake za kiuchunguzi lakini uzoefu wa Mabunge ya wenzetu pamoja na Jumuiya zao zikiwemo SADCOPAC na AFROPAC zinatenganisha utendaji wa Mihimili ya nchi. kwa vile Muhimili wa Serikali kupitia Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali umeshakamilisha majukumu yake, Muhimili mwengine (Baraza la Wawakilishi) ambao ndio chombo kinachowakilisha matakwa ya wananchi unatakiwa ufuatilie tuhuma zilizotolewa na Mdhibiti na kuishauri Serikali nini inatakiwa ikifanye.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha nidhamu za kazi, Kamati ya PAC imebaini kuna baadhi ya watendaji au Taasisi hushindwa kutoa mashirikiano stahiki zinapofika Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi kama inavyotakiwa kutolewa kwa Muhimili wa nchi kama huu katika Mataifa mengine.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mnasaba huo, tunaiomba Serikali kuileta mbele ya Baraza lako Tukufu, Sheria ya Kuanziasha Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar ili iweze kupitiwa na hatimae kufanyiwa marekebisho yatakayohakikisha misingi ya Utawala Bora inaimarishwa zaidi katika Mihimili yote nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya PAC haikuridhishwa na majibu ya udanganyifu yanayokuwa yanatolewa na baadhi ya Watendaji walioaminiwa

kupewa jukumu adhimu na muhimu la kutoa huduma kwa wananchi wetu. Kamati imeligundua hili ilipokuwa Mkoa wa Kaskazini Pemba ikipitia hoja ya Taarifa za mapato na kuelezwa kwamba mapato ya Taasisi hiyo yamepungua kwasababu ya kulitokea Mdhamini aliyewalipia fedha maskini moja kwa moja katika Afisi Kuu ya Usajili wa Matukio ya Kijamii. Hivyo, fedha hizo hawakuweza kuzipata.

**Mheshimiwa Spika,** maelezo hayo hayakuwa ya ukweli na sahihi kwani Kamati yetu ilifanikiwa kukutana na Uongozi wa Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii katika Makao Makuu yao siku ya tarehe 10/2/2023 na kuelezwa kwamba hakuna mapato yaliyolipwa na Mdhamini yeyote kwa huduma za usajili wa vyeti kwa watu waliokuwa hawakusajiliwa awali (late registration). Kwa mnasaba huo, Watendaji wa Mkoa waliidanganya Kamati yako kwa kuipatia majibu yasiyokuwa sahihi na yenye uhakika wa kile wanachokijibu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inawaomba Wasimamizi Wakuu wa Taasisi za Serikali ikiwemo Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kuwa makini na majibu yanayotolewa na watendaji wao na kuyafuatilia kwa karibu ili kubaini kwamba kwa kiasi gani yanakuwa sahihi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa uchunguzi wa **Ripoti ya Ukaguzi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo**, ni ukweli usofichika kuwa Miradi inayotekelezwa kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ikiwemo Miradi ya Maji, Elimu na ujenzi wa Miundombinu ya barabara na umeme inawasaidia Wananchi wengi na kuwaondolea kero mbali mmbali zinazowakabili. Hata hivyo, katika uchunguzi wa Miradi ya Mfuko wa Jimbo Kamati imebaini dosari kadhaa zikiwemo:-

1. Baadhi ya Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa (Halmashauri, Mabaraza ya Mji na Manispaa) kutokuwa Makatibu wa Kamati za Mfuko wa Maendeleo ya Majimbo kama inavyoelekeza Sheria namba 4 ya mwaka 2012. Hali hiyo imejitokeza zaidi katika Majimbo mengi ya Unguja. Aidha kwa baadhi Majimbo ya nayowashirikisha Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kumekuwa na hali kutofautiana baina ya Wenyeviti na Wakurugenzi wa Serikali ya Mitaa husika.
2. Uchache wa fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kulingana na changamoto na mahitaji yaliyopo katika Majimbo.
3. Utunzaji mbaya wa kumbukumbu za Miradi ya Maendeleo ya Jamii inayotekelezwa na baadhi ya Kamati za Mfuko.
4. Majimbo yanayopakana kutokuungana pamoja kutekeleza Miradi mikubwa ya Maendeleo kwa pamoja kama inavyoelekezwa na Sheria.
5. Kuwepo Kwa Miradi mingi ambayo haiwezi kutekelezeka kwa kipindi kifupi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Wenyeviti wa Kamati za Mfuko wa Jimbo ni Wajumbe wa Baraza lako Tukufu, ni matumaini ya Kamati ya PAC kuwa

Viongozi hawa kwa kushirikiana na Serikali watatathimini ufanisi wa utekelezaji wa Miradi ya Mfuko wa Jimbo na watathmini Sheria na miongozo inayohusika kisha kuchukua hatua.

**heshimiwa Spika,** kwa ujumla mambo yote yaliyobainishwa na Kamati zikiwemo dosari mbali mbali za taratibu za kifedha na Ununuzi pamoja na mapendekezo ya Kamati yamefafanuliwa kwa kina katika Hoja mahsusi zinazozihusu Wizara na Taasisi mbali mbali za Serikali na Majimbo kama zinavyoonekana katika Ripoti yetu. Ni matarajio ya Kamati hii kuwa Serikali itazifanyia kazi kasoro zote zilizobainishwa na Kamati kwa kuyatekeleza mapendekezo yaliyotolewa, kwa maslahi ya nchi hii.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia**,** naomba kwa namna ya pekee kabisa kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu kuwasilisha muhktasari huu wa Ripoti ya Kamati ya PAC kwa mwaka 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa kazi za Kamati ya PAC zinatekelezwa na Wajumbe wa Kamati kwa usaidizi mkubwa wa Sekretarieti inayojumuisha Makatibu wa Kamati na Wakaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**,** hivyo basi kwa heshima kubwa, naomba kutoa shukrani maalum na pongezi za dhati kwa Wajumbe wote wa Kamati ya PAC na Sekretarieti ya Kamati kwa kazi kubwa waliyoifanya na umakini wao wa hali ya juu waliouonesha wakati wote wa utekelezaji wa majukumu mazito ya Kamati, hadi leo hii tukamudu kuwasilisha Ripoti hii.

**Mheshimwa Spika**, kutokana na umuhimu huo, naomba kuwataja Wajumbe na Sekretarieti hiyo ya Kamati kama ifuatavyo:-

| **Nam** | **Jina Kamili** | | **Cheo/Wadhifa** |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Juma Ali Khatib | **-** | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Salha Moh'd Mwinjuma | **-** | Makamo Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Mihayo Juma N'hunga | **-** | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Maryam Thani Juma | **-** | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Sulubu Kidongo Amour | **-** | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Suleiman Haroub Suleiman | **-** | Mjumbe |
| 7. | Ndg. Maryam Haji Ali | - | Katibu |
| 8. | Ndg. Said Khamis Ramadhan | - | Katibu |
| 9. | Ndg. Nassor Mdachi Mwinyi | - | Mkaguzi - Ofisi ya Mdhibiti - (Unguja) |
| 10. | Ndg. Aley Mohamed Abeid | - | Mkaguzi - Ofisi ya Mdhibiti - (Unguja) |
| 11. | Ndg. Mussa Kadir Mussa | - | Mkaguzi - Ofisi ya Mdhibiti - (Unguja) |
| 12. | Ndg. Muhamad Saleh Juma | - | Mkaguzi - Ofisi ya Mdhibiti - (Pemba) |
| 13. | Moh'd Suleiman Amour | - | Mkaguzi - Ofisi ya Mdhibiti - (Pemba) |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya PAC inatambua mchango wa Taasisi mbali mbali za Serikali zikiwemo Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Ofisi ya Uratibu wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo pamoja na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutokana na mchango mkubwa walioutoa kwa Kamati yetu. Tunaziomba Taasisi hizo ziendelee kufanyakazi bega kwa bega na Kamati ili kuhakikisha fedha za mapato na Matumizi ya Serikali yetu zinatumika kwa uadilifu na kwa majibu wa Sheria za nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho, naomba kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza pamoja na Kamati yangu ya PAC kwa kuniamini na kuniruhusu kwa roho moja kuuwasilisha Muhtasari huu mbele ya Baraza hili Tukufu. Aidha, ninawaomba Wajumbe wote waijadili, watoe mapendekezo yao na hatimae waipitishe Ripoti hii ya Kamati ya PAC ili ifikapo Septemba, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango aje kutupatia Majibu yake mwezi Septemba kama inavyoelekezwa na Kanuni za Kudumu ya Baraza, Toleo la 2020.

Mheshimiwa Spika, tunawatanabahisha Watendaji wa Wizara za Serikali kwamba pamoja na mambo mengine, Kamati yetu itaendelea kuyafuatilia kwa karibu majibu waliyoyawasilisha mbele ya Kamati kuhusiana na utekelezaji wa Mapendekezo ya Ripoti iliyopita kwa lengo la kutambua utekelezaji halisi wa Serikali ili kuimarisha uwajibikaji na usimamizi wa mapato na nidhamu ya matumizi ya rasilimali za Umma kwa maendeleo endelevu ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kuwasilisha hayo machache kati ya mengi yaliyomo ndani ya Ripoti yetu.

**Mhesimiwa Spika, NAOMBA KUTOA HOJA**.

……………………

**JUMA ALI KHATIB**,
Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti
Hesabu za Serikali,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**